

**SALAMU ZA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) DKT. MUSSA KISSAKA,
KWA KWA KATIBU MKUU KIONGOZI DKT. MOSES
MPOGOLE KUSILUKA, WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA
6 CHA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC – JIJINI
ARUSHA, FEBRUARI 17, 2025**

Mhe. Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka; Katibu Mkuu Kiongozi

Ndugu Mululi Mahendeka; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Ikulu,

Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya

***Mhandisi Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali
Mtandao (e-GA),***

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,

Viongozi wa Dini,

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mhe.. Mgeni Rasmi;

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa zawadi ya afya njema aliyotujaalia na ukarimu wake wa kutukutanisha hapa leo, kwa ajili ya kufungua Kikao Kazi hiki cha 6 cha Serikali Mtandao.

Kipekee, napenda kukushukuru **Katibu Mkuu Kiongozi Dkt. Moses Kusiluka**, kwa kuitikia wito wetu na kukubali kushiriki nasi katika ufunguzi wa Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao. Tunatambua majukumu yako mazito ya kitaifa, na tunaithamini sana heshima uliyotupa kwa kutenga muda wako na kuwa nasi hapa leo. Karibu sana!

Kwa heshima kubwa, napenda kuwakaribisha washiriki wote katika Kikao Kazi hiki, kilichoandaliwa kwa lengo la kuendeleza juhudi za pamoja za kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma za Serikali kwa wananchi.

Kwa niaba ya Bodi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), napenda kuwashukuru wadau wote mlioitikia wito wetu na kushiriki kikao hiki. Ushiriki wenu unaonesha dhamira ya pamoja ya kuijenga Tanzania ya kidijitali yenye mifumo salama, shirikishi na inayozingatia mahitaji ya mwananchi.

Mhe. Mgeni Rasmi;

Kikao hiki kinawakutanisha viongozi wa taasisi za umma, wataalamu wa TEHAMA, sekta binafsi na wadau wengine wa Serikali Mtandao kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujadili mafanikio na changamoto, na kuweka

mikakati ya pamoja ya utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao.

Tunatambua kuwa, licha ya jukumu la kisheria la e-GA la kuratibu na kusimamia jitihada za Serikali Mtandao, mafanikio ya ajenda hii yanahitaji mshikamano na ushirikiano wa karibu wa wadau wote, kuanzia hatua za upangaji hadi utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA katika taasisi zote za umma. Ndiyo maana kikao hiki ni jukwaa muhimu la kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika kuijenga Serikali ya Kidijitali.

Mhe. Mgeni Rasmi;

Kupitia majadiliano ya kikao hiki, tunatarajia kupata maazimio yatakayosaidia kuboresha huduma za serikali mtandao, kuongeza uwazi na ufanisi katika utendaji kazi, na utoaji wa huduma bora zaidi kwa wananchi kupitia TEHAMA.

Kwa mara nyingine tena, napenda kuwakaribisha washiriki wote na kuwahakikishia kuwa e-GA itaendelea kuwa mshirika wenu wa karibu katika safari ya kuijenga Serikali ya Kidijitali.

Karibuni sana!

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

“Kwa pamoja tuijenge Serikali Mtandao kwa vitendo.”